# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

## MASWALI YAULIZWAYO MARA KWA MARA

**Swali 1.** **Nini tofauti ya Mfumo wa utangazaji wa Dijitali na mfumo wa utangazaji wa analojia ambao unatumika kwa sasa?**

Jibu

Tofauti ya mifumo hii miwili,(analojia na dijitali) iko kwenye usafirishaji wa mawimbi ya sauti na picha. Kwa asilia mawimbi ya sauti au ya picha yako kwenye mfumo wa analojia. Mawimbi yaliyo kwenye mfumo wa analojia yanaposafirishwa mbali kwa msikilizaji/mtazamaji yameonyesha kupoteza ubora wa sauti na picha. Mawimbi yanapobadilishwa kutoka mfumo wa analojia kwenda dijitali yanaposafirishwa kwenda mbali yameonyesha kuwa na ubora wa sauti na picha.

Mchoro wa mawimbi ya Analojia na Digitali



**Swali 3. Kwa nini tunahama kutoka mfumo wa utangazaji kwa kutumia teknolojia ya analojia kwenda katika mfumo wa utangazaji kwa kutumia teknolojia ya dijitali?**

Jibu

Sababu kubwa ni faida zilizoko kwenye matumizi ya mfumo wa dijitali kulinganisha na mfumo wa analojia. Faida hizo ni kama ifuatavyo:

i. Ubora wa sauti na picha;

ii. Vifaa vya kuhifadhi habari (CD, VCD, DVD) ni vidogo na huifadhi habari nyingi ukilinganisha na tape recorder na santuri ambazo ziko kwenye mfumo wa analojia;

iii. Matumizi bora ya masafa. Kwa mfano chaneli moja ya analojia hutumiwa na kituo kimoja cha utangazaji wakati kwa mfumo wa dijitali chaneli moja hutmiwa na vituo zaidi ya kumi;

iv. Mitambo ya kurusha matangazo kutumia nguvu ndogo ya nishati;

v. Kuwepo kwa luninga za mkononi (Mobile TV) kwenye mfumo wa dijitali na faida nyinine nyingi;

**Swali 4. Nini Tofauti kati ya Utangazaji wa Televisheni kwa kutumia miundo mbinu ya ardhini (Terrestrial) na utangazaji wa kutumia satelite**

Jibu

Tofauti kati ya utangazaji unaotumia mitambo ya ardhini (Terrestrial) na utangazaji wa kutumia satellite ni kwamba Utangazaji kwa kutumia miundo mbinu ya ardhini unatumia minara na mitambo ya kurushia matangazo (Transmmitters) iliyosimikwa ardhini. Kwa kupokea matangazo ya mitambo hii mtazamaji na msikilizaji hupokea matangazo kwa njia ya antenna zinazofungwa juu ya nyumba au ndani.

Utangazaji wa satelaiti hutumia mitambo ya kurushia matangazo amabayo husimikiwa angani na kurusha matangazo ambayo humfikia mtumiaji kwa njia ya madishi au nyungo zinazofungwa mahali ambapo hakuna kizuizi kwa mawimbi (Masafa) yatokayo kwenye satelaiti. Ukubwa wa madishi haya hutegemeana na teknojia ya mawimbi yanayotumika.

**Swali 5 .** **Nini Maana ya mfumo wa utangazaji kwa kutumia teknolojia ya Dijitali**

Jibu

Ni urushaji wa Matangazo ya Televisheni kwa kutumia teknolojia ambayo imeonyesha kuwa na faida nyingi ukilinganisha na mfumo wa sasa unaotumia teknolojia ya analojia. Utangazaji kwa kutumia mfumo wa dijitali umeonyesha kutopoteza ubora wa picha na usikivu.

**Swali .5** **Je, mabadiliko haya yametokea sehemu nyingine ulimwenguni?**

Jibu

Ndio. Mabadiliko haya yameridhiwa na nchi zote duniani, Bara la Marekani na Ulaya yalianza mchakato huu wa uhamaji kutoka mfumo wa analojia kwenda dijitali mwanzoni mwa mwaka 2000. Bara la Afrika na baadhi ya nchi za mashariki ya kati zilifanya uamuzi wa uhamaji kutoka mfumo wa analojia kwenda dijitali mwaka 2006.

**Swali 6.** **Je nitahitaji ungo wa satelaiti kupokea matangazo ya mfumo wa utangzaji wa digitali unaotumia mitambo ya kurushia matangazo iliyosimikwa ardhini ( Terrestrial)?**

Jibu

Hapana. Ungo wa satelaiti ni kwa ajili ya mfumo wa matangazo unaotumia mitambo ya kurushia matangazo yalioko angani kwenye satellite.

**Swali7.** **Je nitahitaji antenna mpya kupokea matangazo ya dijitali?**

Jibu

Hapana – Antena unayotumia sasa kwa ajili ya kupokea matangazo ya mfumo wa analojia iliyofungwa juu ya nyumba au iliyoko ndani yaweza kutumika. Hata hivyo unashauriwa kuwasiliana na mtoa huduma ili aweze kukupa ushauri unaofaa kwa matumizi ya kupokea matangazo kwa kuzingatia eneo la kijiografia unapoishi.

**Swali 8. Je zaidi ya luninga na antenna , nitahitaji vifaa zaidi kupokea matangazo ya dijitali?**

Jibu

Ndiyo – Kwenye luninga zetu za analojia tunahitaji kifaa cha ziada ili kuweza kupokea matangazo yanayorushwa kwa mfumo wa digitali. Kifaa hicho kinaitwa king'amuzi (Decoder). King'amuzi kinatumika na luninga inayopokea matangazo ya analojia. Kazi ya king'amuzi ni kubadilisha mawimbi ya mfumo wa dijitali na kuwa kwenye mawimbi ya mfumo wa analojia.

**Swali 9. Nini maana ya King'amuzi?**

Jibu:

King'amuzi ni kifaa kinachotumika kupokea matangazo yanayorushwa kwa mfumo wa digitali ili yaonekane na kusikika katika luninga za analojia.

King'amuzi

(Set-Top-Box)



**Swali 10 Nini umuhimu wa King'amuzi katika mfumo wa digitali?**

Jibu:

King'amuzi kinahitajika ili matangazo yanayorushwa katika mfumo wa digitali yaonekane na kusikika kwenye luninga za analojia (hii ni pamoja na picha na sauti). Bila kifaa hiki, mawimbi yaliyobadilishwa kutoka mfumo wa dijitali hayawezi kuonekana kwenye runinga za analojia.

**Swali 11. Ili mtazamaji aweze kupokea na kuona matangazo yanayorushwa kwenye mfumo wa dijitali ni lazima kulipia matangazo hayo?**

Jibu:

Hapana. Matangazo ambayo yamekuwa yakionekana bila kulipia kwenye mfumo wa analojia yataendelea kutolewa bure. Matangazo haya ya luninga ni kama yale yanayorushwa na vituo vya TBC1, Channel Ten, Star TV, ITV n.k. Isipokuwa kuna matangazo ya luninga yanayo rushwa kutoka vituo mbalimbali ambayo ni ya kulipia. Ikiwa mtazamaji atapendelea kuona matangazo hayo itabidi kuwasilana na mtoa huduma ili aweze kujiunga na huduma ya malipo yakiwa kwenye mfumo wa kapu (**bouquet**).

**Swali 12. King'amuzi kitauzwa kwa bei gani?**

Jibu

Bei ya king'amuzi inategemea ushindani kwenye soko. Hata hivyo bei ya kingamuzi kwa sasa ni kati ya shilingi za kitanzania 70,000 mpaka 100,000. Gharama zinaweza zikashuka kutegemea ongezeko la watumiaji wa vifaa hivyo kwenye soko.

**Swali 13. Je kama nina king'amuzi kinachopokea matangazo yanayorushwa kutoka kwenye satellite (DSTV/ZUKU) naweza kukitumia kwa kupokea matangazo yanayorushwa na mitambo iliyosimikwa ardhini(Terrestrial) au nitahitaji king'amuzi kingine?**

Jibu

Ndiyo, utahitaji king'amuzi kingine. DSTV/ZUKU ni huduma ya satelaiti. Kama ilivyoelezwa mwanzo, mawimbi ya satelaiti yanatumia mfumo tofauti wa masafa pamoja na mfumo wa kiufundi hivyo kumlazimu mtumiaji kuwa na king'amuzi tofauti kupokea matangazo ya mfumo wa digital yanayo rushwa na mitambo iliyosimikwa ardhini(Terrestrial).

**Swali 14. Je king'amuzi kinapatikana au kuuzwa wapi?**

Jibu

King'amuzi kitapatikana kwa makampuni yaliyopewa leseni na Mamlaka ya Mawasiliano. Leseni hiyo ni kwa ajili ya kuagiza na kuuza vifaa vya mawasiliano ikiwa ni pamoja na utangazaji.

**Swali 15. Je ni makampuni mangapi yaliyopewa leseni ya kujenga miundombinu ya kurusha matangazo ya dijitali?**

Jibu

Mpaka sasa Mamlaka imetoa leseni kwa makampuni matatu yafuatayo:

i. Star Media (T) Limited

ii. Agape Associate Limited

iii. Basic Transmission Limited

**Swali 16. Nini Kazi ya Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kwenye kutoa huduma za matangazo ya luninga kwenye mfumo wa dijitali?**

Jibu

Kazi kubwa ya Mamlaka ya Mawasiliano ni kusimamia na kuratibu zoezi zima la uhamaji kutoka utangazaji wa luninga wa mfumo wa analojia kwenda mfumo wa dijitali. Vile vile kutoa leseni kwa watoa huduma wa miundo mbinu ya dijitali, waagizaji na wasambazaji wa vifaa vya dijitali(Vingamuzi) na vituo vya utangazaji kwenye mfumo wa dijitali.

**Swali 17. Je nikiwa na kingamuzi naweza kupokea matangazo ya dijitali mahali popote nchini?**

Jibu

Hapana. Utapokea matangazo kwenye mfumo wa dijitali ikiwa tu eneo ulipo kuna mtambo wa ardhini (terrestrial) wa kurushia matangazo kwenye mfumo wa dijitali. Mitambo hii inaweza ikasafirisha mawimbi kama kilomita 50 mpaka 80 kutegema nguvu ya mtambo.

**Swali 18. Je king’amuzi kinafungwa namna gani hadi kipate kufanya kazi?**

Jibu

King’amuzi kinahitaji maelekezo ya kitaalamu ili kiweze kufanya kazi vizuri. Hakikisha unwasilana na muuzaji ili uweze kupata msaada katika ufungaji wa king’amuzi hiki.

**Swali 19. Je nitahitaji kununua luninga mpya kwa ajili ya matangazo ya digitali?**

Jibu

Hapana, luninga zote za analojia zinaweza kupata matangazo ya dijitali kwa kutumia king'amuzi.

**Swali 20. Lini itakuwa mwisho wa kupata matangazo ya analojia?**

**Jibu**

Kwa Tanzania na nchi za Afrika Mashariki, mwisho wa kurusha matangazo ya analojia ni tarehe 31 Disemba, 2012. Baada ya hapo wale wote wasio na ving'amuzi hawataweza kuona matangazo ya televisheni.